

Kama ni Mungu ndiye kaumba zao la Bangi kwanini tena iwe dhambi
kuitumia??

Swali: Biblia inasema tumepewa mboga za majani kuwa chakula chetu, na Bangi pia ipo mionganoni mwa zao la mboga za majani...sasa kwanini iwe dhambi kulitumia kama mboga au kiburudisho cha kusisimua (*kuvuta*) na ilihali ni Mungu mwenyewe ndio kaumba?

Jibu: Turejee..

Mwanzo 9:3 "Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu, kama nilivyowapa MBOGA ZA MAJANI, kadhalika nawapeni hivi vyote".

Ni kweli maandiko hayo yanathibitisha ulaji wa mboga, lakini si mboga zote!.. Tukisema kila mboga iliyopo kondeni tumepewa tule, tutakuwa hatujayaelewa vizuri maandiko kwasababu kuna mboga nyingi sana ambazo sumu!, ambazo zinamwonekano mzuri lakini hazifai kwa chakula... na Mungu hawezi kumpa ruhusa Mtu wake aliyemuumba, ale **SUMU!**..

Zipo mboga kwaajili ya chakula cha wanadamu, nyingine kwaajili ya

Kama ni Mungu ndiye kaumba zao la Bangi kwanini tena iwe dhambi
kuitumia??

wanyama na hazifai kwa wanadamu... vile vile zipo mboga zisizofaa kwa chakula cha wanadamu na wanyama... Mboga hizo zinabaki tu kwa utukufu wa Mungu, au kwaajili ya urembo, mfano wa mboga hizo ni **MAUA.**

Kuna Maua ambayo yana mwonekano mzuri sana lakini ni SUMU kali sana, mfano wa hayo ni kama haya yanavyoonekana hapa chini.



Hayo ni mfano wa Mboga, lakini si kwaajili ya kula bali kwaajili ya urembo tu.. yameumbwa na Mungu kwa lengo hilo, hivyo mtu akila hayo anaweza kupata madhara makubwa ya kiafya au hata kifo.

Vile vile na Bangi, inaweza kuwepo katika kundi hilo la MAUA, kama

Kama ni Mungu ndiye kaumba zao la Bangi kwanini tena iwe dhambi
kuitumia??

itatumika kwa urembo si vibaya, lakini kwa matumizi mengine ya ndani
ya mwili wa binadamu ni hatari.

Kwahiyo si kila kilicho halalishwa basi kinafaa kwa matumizi yote..
hapana!.. Mboga zimehalalishwa lakini si kwa matumizi ya chakula tu,
ndivyo maandiko yanavyotufundisha..

*1Wakorintho 10:23 “Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vifaavyo.
Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vijengavyo”.*

Kwahiyo ulaji, au uvutaji wa Bangi ni dhambi kibiblia, vile vile matumizi
ya tumbaku kula au kuvuta ni dhambi, kwani miili yetu ni hekalu la
Roho Mtakatifu, na tena maandiko yanasema mtu akiliharibu hekalu hilo
Mungu naye atamharibu mtu huyo (*Soma 1Wakoritho 3:16-17 na
1Wakorintho 6:19*).

Na Bangi inaharibu ufahamu wa mtu, ambao ndani yake kunazalika
hasira, kutokujali, vurugu, matukano, mauaji, uasherati na mambo yote
mabaya..

Hivyo Bangi ni haramu, vile vile tumbaku na mazao mengine yaletayo

Kama ni Mungu ndiye kaumba zao la Bangi kwanini tena iwe dhambi
kuitumia??

matokeo kama hayo.

Bwana atusaidie.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako
bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge
na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

[Nyungu ni nini kibiblia?\(Ayubu 41:20,31, Waamuzi 6:19\)](#)

MTINI, WENYE MAJANI.

Kama ni Mungu ndiye kaumba zao la Bangi kwanini tena iwe dhambi
kuitumia??

JE UNAZAA MATUNDA NA KUWAPONYA MATAIFA?

WENGINE WANAKESHA KWAAJILI YAKO.

**Nini maana ya mmoja alikufa kwaajili ya wote hivyo walikufa
wote? (2Wakorintho 5:14)?**

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp